# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
## CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - ARUSHA

**VTC/AR/AB/VOL II /03/01** **Tarehe: 20 Julai, 2026**

# TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA ZA MKATABA

Chuo cha VETA Arusha ni miongoni mwa vyuo vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya ufundi stadi (VETA); Chuo kipo katika Wilaya ya Arusha, Kata ya Muriet, Mtaa wa Bondeni. Pamoja na majukumu ya kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa ngazi ya kwanza hadi ya tatu (NTA Level I hadi III) Chuo kinatoa Mafunzo ya Udereva wa Magari katika Ngazi mbalimbali. Katika kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi VETA Arusha inawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi ya kazi kwa masharti ya ajira za mkataba ya miaka mitatu (3) kama ifuatavyo:

### 1. MKUFUNZI WA UDEREVA (DRIVER INSTRUCTOR)- (NAFASI 2)

### 1.1 KAZI NA MAJUKUMU

(i) Kufundisha udereva kwa ngazi ya udereva wa awali, udereva wa magari ya abiria na maroli.

(ii) Kuandaa matokeo ya wanafunzi walioshiriki mafunzo kwa awamu (intake) husika,

(iii) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;

(iv) Kubaini changamoto au matengenezo ya gari na kutolea taarifa;

(v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari;

(vi) Kufanya usafi wa gari.

(vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

**i.** Awe na cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu (3) pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyompatia sifa ya kupata madaraja husika yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

**ii.** Awe amehitimu mafunzo ya ukufunzi wa madereva (Driving Instructor) daraja A (**Awe na smart card)**

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA: VETAS 2

### 1.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

iii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

v. “Testmonial”, ‘‘Provisional Results “, “Statement of results “, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.

vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

viii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 31 Julai, 2026

ix. MUHIMU: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, maombi yatumwe kupitia barua pepe **arushavtc@veta.go.tz** na anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**MKUU WA CHUO,**
**VETA ARUSHA,**
**S.L.P 509,**
**ARUSHA.**

Kwa niaba ya, ***CHUO CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI – ARUSHA***

Happiness Bwire Nyamaka
**MKUU WA CHUO**

**Nakala: Mkurugenzi wa Kanda,**
**VETA Kanda ya Kaskazini,**
**S.L.P 1738, MOSHI.**